
# I. SALA YA SIKU THELATHINI KWA MT. YOSEFU.




- *Kwa ajili ya nia yoyote ya dhati.*
- *Siku hizi thelathini zaweza kuwa zozote zile katika mwaka.*
- *Kwa heshima ya miaka thelathini aliyoishi Mt. Yosefu.*

*"Mt. Yosefu usiye na lawama, utuongoze kwenye ulinzi wako mwema kuwa huru dhidi ya hatari zote".*

Ewe uliyebarikiwa na mtukufu milele Yosefu, baba mwenye huruma na mpendevu, na rafiki msaidizi wa wote walio katika huzuni! Wewe ni baba mwema na mlinzi wa yatima, mlinzi wa wasio na ulinzi, mlezi wa wale walio na mahitaji na wenye huzuni. Liangalie kwa wema wako ombi langu. Dhambi zangu zimenielemea, pia Mungu wangu haridhishwi nami kwa haki, hivyo nazungukwa na ukosefu wa furaha. Kwako wewe, mlezi wa familia Takatifu, naukimbilia msaada na ulinzi wako.

Nisikilize, nakusihi, kwa kujali kwako kwa kibaba, kwa sala yangu ya dhati, na uniombee niupate upendeleo niuombao.

Ninaomba ombi hili kutokana na huruma isiyo na mipaka ya mwana wa milele wa Mungu, ambayo ilimsukuma kuchukua hulka yetu na kuzaliwa katika ulimwengu wetu wa huzuni.

Ninaomba kutokana na uchovu na mateso yako uliyoyavumilia pale ulipokosa si tu hifadhi kwenye nyumba ya wageni Bethlehemu kwa ajili ya Bikira Mtakatifu, bali pia nyumba ambapo Mwana wa Mungu angezaliwa. Hapo, ulipokataliwa pote, ulilazimika kuruhusu Malkia wa mbingu kumzaa mwokozi wa ulimwengu katika pango.

Ninaomba hili kwa upendo na nguvu ya jina lake takatifu Yesu ambalo ulimpatia Mwana mwabudiwa.

Nakuomba hili kutokana na yale mateso yako makali ambayo uliyasikia kutokana na unabii wa Simoni Mtakatifu, ambaye alitabiri kuwa Mtoto Yesu na Mama yake mtakatifu watakuwa wahanga wa dhambi zetu na  upendo wao mkubwa kwetu.

Nakuomba hili kutokana na huzuni na mateso yenye maumivu ya roho pale ambapo malaika alipotangaza kwako kwamba maisha ya Mtoto Yesu yalikuwa yanatafutwa na maadui zake. Kutokana na mpango wao mwovu, ulikimbia pamoja naye na Mama yake Mwenyeheri kuelekea Misri. Nakuomba hili kutokana na mateso, uchovu, kazi na safari hiyo ndefu na yenye hatari.

Nakuomba  hili kutokana na kujali kwako kote kumlinda Mtoto Mtakatifu na Mama yake asiye na doa katika safari yako ya pili, pale ulipoagizwa kurudi nchini kwako. Ninakuomba hili kwa njia ya maisha yako ya Amani ukiwa Nazarethi ambako ulikutana na furaha na huzuni nyingi.

Ninakuomba hili kutokana na dhiki kuu uliyoipata pale Mtoto wako mwabudiwa alipopotea toka kwako na kwa Mama yake kwa siku tatu. Ninakuomba hili kutokana na furaha ya kumkuta Hekaluni, na kwa faraja ambayo uliipata Nazarethi, wakati ulipoishi pamoja na Mtoto Yesu. Nakuomba hili kwa kujitoa kwake kwa ajabu kwako kwa utii wake wa dhati.

Ninakuomba hili kutokana na upendo kamili na kufungamana ulikoonesha katika kukubali agizo la kiungu kuondoka kutoka maisha haya, na kutoka katika uwepo wa Yesu na Maria. Nakuomba hili kwa furaha ambayo ilijaza roho yako, pale ambapo Mwokozi wa ulimwengu, alishinda kifo na kuzimu, na kuingia kutamalaki uflame wake na kukuongoza wewe humo kwa heshima ya pekee.

Ninakomba hili kwa njia ya kupalizwa mbinguni wa utukufu kwa Mama, na kwa njia ya furaha isiyo na mwisho uliyonayo mbele ya uwepo wa Mungu.
Ee baba mwema! Nakusihi kutokana na mateso, huzuni na furaha, unisikilize na kuniombea nipate hili niliombalo……………………… (*taja ombi la pamoja kwa maombezi ya Mtakatifu Yosefu wagonjwa wa corona wapate uponyaji, kwa maombezi ya Mt. Yosefu Familia zetu zikingwe na janga la Corona, …ongeza hitaji lako* km nia Binafsi).

Waombee wafanikiwe wale walioomba sala zako, katika yale yote yenye manufaa katika mpango wa Mungu. Mwishowe mpendwa wangu, mlezi na baba, uwe nami na wale wote ambao ni wapendwa katika muda wetu wa mwisho, ili tuweze kuimba milele sifa za Yesu, Maria na Yosefu. **Amina.**

## II. NOVENA KWA MT. YOSEFU.

*(Sala hii inapaswa kusaliwa mwishoni mwa uchaji wa siku).*

Mt. Yosefu, mimi mtoto wako nisiye na thamani, nakusalimu. Wewe ni mlinzi na mwombezi mwaminifu wa wote ambao wanakupenda na kukuheshimu wewe. Unafahamu kwamba nina Imani thabiti kwako, na kwamba baada ya Yesu na Maria, naweka matumaini yangu ya wokovu kwako, kwani wewe una uwezo maalumu mbele ya Mungu na kwamwe huwezi kumtelekeza mtumishi wako mwaminifu. Hivyo kwa unyenyekevu ninakuomba na kujiweka mikononi mwako pamoja na

wote ambao ni wapendwa wangu na vyote ambavyo ni vyangu, kwa maombezi yako. Nakusihi, kwa upendo wako kwa Yesu na Maria, usiniache wakati wa uhai wangu na unisaidie saa ya kufa kwangu.

Mtukufu Mt. Yosefu, mume wa Bikira asiye na doa, uniombee nipate akili safi, nyenyekevu, karimu na yenye kujitoa kikamilifu kwa dhamiri ya Mungu. Uwe kiongozi wangu, baba yangu, mfano katika maisha ili niweze kustahili kufa kama wewe mikononi mwa Yesu na Maria.

Mpendwa Mt. Yosefu mfuasi mwaminifu wa Yesu Kristo, naunyanyua moyo wangu kwako kuomba maombezi yako yenye nguvu ili kupata toka kwa Moyo wa kiungu wa Yesu neema zote za lazima kwa ajili ya mapambano yangu ya kiroho ya ustawi wa maisha ya kidunia, hasa neema ya kifo cha furaha na mema maalumu ambayo ninaiomba sasa…… (*taja ombi lako*).

Mlinzi wa Neno Mwilika, nina uhakika kwamba sala zako kwa niaba yangu zitasikilizwa kwa ukarimu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. **Amina.**

## III. SALA YA ZAMANI SANA KWA MT. YOSEFU KWA AJILI YA KIFO CHEMA.

Ee, Mt. Yosefu, ambaye ulinzi wako ni mkubwa sana, wenye nguvu, na wa haraka mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Naweka kwako ninayoyapenda na kuyatamani. Ee, Mt. Yosefu, nisaidie kwa maombezi yako yeye nguvu, na nijalie kutoka Mtoto wako wa kiungu, Baraka zote za kiroho, kwa njia ya Yesu Kristo, Bwana wetu. Ili kwamba, baada ya kusaidiwa na nguvu ya kimbingu hapa duniani, niweze kujitoa mwenye kumshukuru na kumheshimu  mpenda Zaidi wa mababa wote.

Ee Mt. Yosefu, kamwe sichoki kukutafakari wewe, na Yesu akiwa amelala mikononi mwako, sithubutu kuwakaribia akiwa amepumzika karibu na moyo wako.

Mkumbatie kwa niaba yangu na busu kichwa chake kizuri kwa niaba yangu na mwombe naye anibusu mimi nitakapovuta pumzi yangu ya `kifo.

Mt. Yosefu, mlinzi waroho zilizo kufani- utuombee.

***REJEA;***


1. Mtakatifu Yosefu Msimamizi wa Kanisa la Ulimwengu. Na; Rozari Hai Mtandaoni
2. Mfahamu Mtakatifu Yosefu, Sala na Novena. Na Pd. Stefano Kaombe


Kuandaliwa na Fortunata R. Masaka